

CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE



MAHAFALI YA KUMI NA TISA (19) KAMPASI YA KIVUKONI, MAHAFALI YA TISA (9) KAMPASI YA KARUME - ZANZIBAR NA MAHAFALI YA PILI (2) KAMPASI YA PEMBA KWA MWAKA 2024

Mkuu wa Chuo anawatangazia wanafunzi waliohitimu masomo yao katika mwaka wa masomo 2023/2024 kwamba Mahafali katika kampasi zake zote tatu yatafanyika kama ifuatavyo; Kampasi ya **Kivukoni jijini Dar es salaam** ambayo ni **Mahafali ya Kumi na TISA** yatafanyika siku ya **Ijumaa tarehe 29 Novemba, 2024**, Kampasi ya **Karume visiwani Zanzibar** ambayo ni **Mahafali ya TISA** yatafanyika siku ya **Jumatatu tarehe 2 Desemba, 2024** na kwa Kampasi ya **Pemba** ambayo ni **Mahafali ya Pili** Mahafali yatafanyika siku ya **Jumatano tarehe 4, Desemba 2024** na kuwa **Mahafali kwa Kampasi zote yataanza saa TATU ASUBUHI (03:00)**.

Wahitimu kwa Kampasi zote wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:

1. Kuchukua Majoho kwa Kampasi ya Kivukoni ni kuanzia **Ijumaa, tarehe 22.11.2024 hadi Alhamisi, tarehe 28.11. 2024**, kwenye ofisi namba 115 – Jengo la Uhuru, **Kampasi ya Karume - Zanzibar majoho yatatolewa kuanzia siku ya Jumatatu tarehe 18.11.2024 hadi siku ya Ijumaa ya tarehe 29.11.2022**, na Kwa Kampasi ya **Pemba Majoho yatatolewa kuanzia tarehe 2.12.2024 hadi 3.12.2024**. Majoho yatatolewa kuanzia **4:00 asubuhi hadi saa 9:00 alasiri** kwa Kampasi zote na kuwa **Majoho hayatatolewa siku ya mahafali**.
2. **MALIPO YOTE YA KULIPIA MAJOHO YALIPWE KWA KUTUMIA MFUMO WA KIELEKTRONIKI (CONTROL NUMBER)**
3. Majoho sharti yarejeshwe Chuoni kabla ya **tarehe 6 Desemba, 2024 kwa Kampasi zote**. Vinginevyo **faini ya shilingi 10,000/=** itatozwa kwa siku kwa yeyote atakayechelewa kurudisha joho hilo.
4. Zoezi la namna ya kupokea vyeti (**rehearsal**) litafanyika **Alhamis, tarehe 28 Novemba, 2024** kuanzia **saa 6.00 mchana** kwa kampasi ya **Kivukoni**, na mahafali yatafanyika katika uwanja wa Mpira **Kampasi ya Kivukoni**. **Kampasi ya Karume-Zanzibar** zoezi hilo litafanyika **Jumapili tarehe 1 Desemba** ,

2024 kuanzia **saa 4:00 asubuhi** katika uwanja wa mahafali Chuoni hapo. Na kwa **Kampasi ya Pemba rehearsal** itafanyika siku ya Jumatatu tarehe 3.12.2024 katika viwanja vya Kampasi ya Pemba Pujin, Chakechake Pemba.

Mhitimu atakayeshindwa kuhudhuria zoezi hilo la rehearsal, HATARUHUSIWA kushiriki katika Mahafali.

5. Kila mhitimu atapaswa kujigharamia usafiri, malazi na chakula.
6. kusanyiko la wahitimu wote yaani **(CONVOCATION)** waliosoma katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere litafanyika katika Kampasi ya Kivukoni jijini Dar es Salaam siku ya **Alhamis, tarehe 28 Novemba 2024** katika Ukumbi mpya wa Mihadhara **(NEW LT)** chuoni hapo kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa sita mchana.
7. **WASHIRIKI WOTE WA MAHAFALI WANATAKIWA KUTHIBITISHA USHIRIKI WAO KATIKA OFISI YA MITIHANI KABLA YA tarehe 27 Novemba, 2024** kwa kupiga simu namba zifuatazo: **0679907412, 0782405552 na 0762020129**

NYOTE MNAKARIBISHWA.

Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere,
S.L.P. 9193,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2820041/ 2820045/ 2820047
Faksi: +255 22 2820816
Barua pepe: rector@mnma.ac.tz